SautiElimu

hakielimu

Toleo la 11
2005
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Elimu itimize mahitaji ya watanzania

Nyanda Shuli, Idara ya Habari, HakiElimu

Lengo la elimu ni kumwandaa mwanafunzi kuishi katika mazingira aliyopo kwa kumpa ufahamu na ujuzi wa kufanya mambo mbali mbali.

Mitaala ni nyenzo muhimu katika ufundishaji kwani inaonyesha masomo anayotakiwa kufundishwa mwanafunzi pamoja na mada zake. Mitaala hufanyiwa mabadiliko ili elimu iendane na wakati. Mabadiliko ya mitaala mara nyingi yanatokana na mahitaji ya watu na sekta mbalimbali katika jamii. Lengo ni kuwawezesha wahitimu waweze kuitumia elimu waliyopata katika kuboresha maisha yao.

Nakumbuka kauli ya Mwalimu Julius Nyerere aliyoitoa mwaka 1967 kuwa: "Elimu inayotolewa na nchi ya Tanzania kwa wanafunzi wa kitanzania sharti itimize malengo ya nchi." Kauli hiyo inatukumbusha kuunda mfumo wa elimu unaoendana na hali halisi nchini. Kwa mfano; sasa kuna uhaba wa ajira, hivyo elimu inayotolewa iwawezeshe wahitimu kujitegemea.

Katika jarida hili, Jacob Massaba wa Kidatu anachangia maoni kuhusu uamuzi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kufuta masomo ya Historia, Jiografia na Uraia katika shule za msingi na kuyaunganisha kuunda somo la Maarifa ya Jamii. Anaeleza kwamba mada za masomo hayo kwa sasa zinafundishwa juu juu kiasi kwamba wanafunzi wanakosa undani wa masomo yaliyounganishwa.

Naye Johansen Kempanju wa Itahwa, Dar es Salaam anaishauri Serikali iboreshe mafunzo ya elimu ya ualimu ili kuendana na mabadiliko ya mitaala. Anatoa mfano wa ugumu wanaopata walimu wengi wa shule za msingi kufundisha somo la Stadi za Kazi.

Sylvester Moses wa Kahama anaishauri Wizara iwape walimu motisha na iboreshe mazingira ya kazi ili wasizikimbie shule zilizoko vijijini. Naye Primu Alphonce wa Dar es Salaam anatahadharisha juu ya madhara ya kufundisha kinadharia bila vitendo. Vile vile walimu katika habari iliyoandikwa na M. Sunday wa Bariadi wanashauri kufutwa kwa matumizi ya daftari la andalio la somo na badala yake watumie daftari la notisi katika kuandaa somo.

Hayo ni baadhi tu ya maoni ya wananchi kwamba elimu inayotolewa ilenge kumwezesha mwanafunzi kujitegemea na kuzalisha pindi amalizapo masomo. Elimu ya aina hiyo ni muhimu ili kupambana na ukuaji wa uchumi na mahitaji ya soko la ajira. Pengine Serikali ingewashirikisha wananchi katika ngazi mbalimbali za uwakilishi kuamua masomo yapi na mada zipi ziwepo kwenye mtaala.

Walimu waandaliwe kufundisha Stadi za Kazi

Johansen Kempanju, Itahwa - Dar es Salaam

Naipongeza Serikali kwa jitihada za kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu nchini. Shule zinaendelea kujengwa na nyingine kukarabatiwa, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinaendelea kutolewa.

Mbali na jitihada hizo, Serikali katika miaka ya karibuni ilibadilisha mtaala katika shule za msingi kwa kuingiza somo la Stadi za Kazi. Serikali pia imegharamia fedha nyingi kwa ajili ya uchapishaji wa vitabu vya wanafunzi na walimu. Vilevile imepanga mada gani ziingizwe katika muhtasari wa somo hilo.

Ili kufanikisha ufundishaji wa somo hilo nashauri Serikali itilie mkazo suala la kuwaandaa walimu wa kufundisha Stadi za Kazi. Walimu wengi katika shule za msingi walimaliza mafunzo kabla mtaala haujabadilika. Sitashangaa kusikia kuwa somo hilo halifundishwi vizuri katika baadhi ya shule. Ni vigumu kwa walimu kufundisha mada kama ufundi saa, ufundi redio au ufundi bomba wakati hata wao wenyewe hawajawahi kufundishwa kutengeneza vitu hivyo.

Lengo la kuanzishwa kwa somo hili lilikuwa ni kuwawezesha wanafunzi wakihitimu elimu ya msingi waweze kujiajiri. Itakuwa vigumu kufikia lengo hilo endapo walimu hawataandaliwa vizuri. Napendekeza Serikali iteue baadhi ya walimu kutoka kila shule wakapate mafunzo ili waweze kufundisha somo hili kwa ufanisi zaidi.

Wadau washirikishwe kubadili mitaala

Jacob Massaba, SLP 98, Kidatu

Mabadiliko ya kuunganisha masomo ya Historia, Jiografia na Uraia na kuunda somo moja la Maarifa ya Jamii yanawapa ugumu wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi wanapojiunga na shule za sekondari.

Somo la Maarifa ya Jamii linagusa mada za masomo yaliyounganishwa kwa ufupi sana. Naamini kuwa masomo hayo ni muhimu yafundishwe kwa undani katika ngazi ya chini. Huo utakuwa ndio msingi wa kuelewa vyema na kuweza kuendelea na masomo hayo katika ngazi ya juu.

Vile vile masomo ya Biashara, Kilimo na Ufundi yaliyoondolewa katika mtaala wa elimu ya sekondari nayo yanaleta utata. Mabadiliko hayo yanawaumiza wanafunzi na walimu waliokuwa wamebobea katika masomo hayo. Tutawezaje kupata wataalam wa biashara na kilimo hapo baadaye? Nini hatma ya walimu wanaofundisha masomo hayo?

Naishauri Wizara ya Elimu na Utamaduni kwamba masomo hayo yaanzie shule za msingi ili wanafunzi waanze kupata uzoefu mapema. Yawezekana mwanafunzi akayapenda akiwa mdogo, na kujikuta akibobea katika fani zinazotokana na masomo hayo. Kuyaondoa kutapunguza nafasi ya watoto kukuza vipaji wakiwa wadogo na kushindwa kujiajiri kwa wale watakaoishia kidato cha nne.

Idadi ya watanzania waliobobea katika fani mbalimbali bado ni ndogo. Kufuta masomo ya Kilimo, Ufundi na Biashara kwa shule za sekondari kunawaondolea wengi uwezekano wa kuipata elimu hiyo baadaye.

Nashauri wadau wa elimu watathmini mabadiliko hayo na kufanya maamuzi kwa manufaa ya wote.

Walimu wapewe motisha kufundisha vijijini

Sylvester Moses, SLP 308, Kahama

Tatizo la upungufu wa walimu nchini linazikumba zaidi shule zilizoko vijijini. Walimu wengi wenye uzoefu hawakubali kufanya kazi vijijini kwa madai kuwa maisha ni magumu na hakuna huduma bora za jamii.

Walimu wengine wanasema kuna tatizo la kutokuwa na nyumba nzuri za kuishi vijijini. Wengine wanadai upatikanaji wa mishahara ni tatizo kwani hulazimika kusafiri ili kufikia vituo vya malipo. Hizo ni baadhi ya kero ambazo zinasababisha walimu wengi wakimbilie mijini.

Kutokana na sababu hizo, yapo maeneo ambayo walimu ni wengi na maeneo mengine yana upungufu mkubwa. Tofauti hii imesababisha uwiano kati ya mwalimu na wanafunzi katika darasa moja kuwa kubwa kwenye baadhi ya mikoa. Kwa hali hiyo, tatizo si kutokuwa na walimu wa kutosha bali ni mazingira yaliyopo na mgawanyo wa walimu.

Wingi wa wanafunzi darasani unaathiri ubora wa elimu kwani mwalimu hawezi kufuatilia maendeleo ya kila mwanafunzi. Imekuwa kawaida sasa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuhitimu bila kuwa na ujuzi, uelewa na ufahamu ambao umetajwa katika mitaala.

Kabla ya kufikiria kuajiri walimu wapya (kama bajeti haitoshi) ni muhimu kufikiria uwezekano wa kuwasambaza walimu waliopo ili kuleta uwiano. Serikali iangalie namna ya kuweka vivutio vitakavyowawezesha walimu kufanya kazi katika maeneo ambayo hawataki kwenda. Huduma kama za usafiri, umeme, maji safi na salama, zahanati, nyumba bora za kuishi, benki na maktaba ni baadhi tu ya vivutio kwa walimu kwenda vijijini.

Serikali ikiweza kuboresha huduma hizo kutakuwa na mgawanyo na uwiano mzuri wa walimu katika shule nchini. Vijijini pia kuna wanafunzi wenye haki ya kupata elimu na walimu mahiri wenye uzoefu.

Ukurasa wa 1

SautiElimu

Toleo la 11
2005
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Barua kwa SautiElimu

Sababu za wanafunzi kutofaulu hizi hapa

Ahmed Muhammed Ahmed, Dar es Salaam

Taarifa zinazotolewa kupitia vyombo vya habari zinaonyesha kuwa ziko baadhi ya shule ambazo kwa miaka mingi hazijafaulisha wanafunzi.

Sababu za wanafunzi kutofaulu ni nyingi. Kwanza, ni walimu kushindwa kuhudhuria vipindi darasani. Kutohudhuria masomo kunasababishwa na uhaba wa walimu unaozikabili shule nyingi hasa zile za Serikali zilizoko vijijini. Utakuta mwalimu amepangiwa kufundisha vipindi vingi na hivyo kushindwa kuhudhuria vingine kutokana na uchovu ama kubanwa.

Mwalimu akiwa na vipindi vingi hawezi kufundisha kwa makini na kufuatilia maendeleo ya kila mwanafunzi. Vile vile si rahisi kwa mwalimu kusahihisha madaftari ya wanafunzi wa madarasa yote anayofundisha.

Pili, wazazi kutofuatilia walichojifunza watoto wao shuleni pia kunasababisha matokeo mabaya. Ni jukumu la wazazi kukagua madaftari ya watoto wao na kuwasaidia kimasomo pindi wanapokuwa nyumbani.

Tatu, ukali wa walimu shuleni pamoja na adhabu ikiwemo ya viboko hujenga hofu kwa wanafunzi. Wanakuwa waoga kuuliza maswali, kutoa hoja na hata kushiriki katika mijadala.

Sababu hizo na nyingine nyingi zinaweza kurekebishwa ikiwa wazazi, walimu na wanafunzi watashirikiana na viongozi katika kutafuta suluhisho kwa pamoja. Kwa mfano, wazazi wenye elimu ya juu wanaweza kujitolea muda wao wa ziada kwa sasa kufundisha baadhi ya masomo katika shule zenye upungufu wa walimu.

Mwisho, nashauri Serikali itimize ahadi ya kuongeza idadi ya walimu katika shule za umma, kwa mujibu wa MMEM. Vile vile walimu walipwe mishahara na mafao yao kwa wakati ili watumie muda mwingi katika kufundisha.

Kufundisha kinadharia bila vitendo ni kudidimiza elimu

Primu Alphonce, SLP 54166, Dar es Salaam

Elimu kwa vitendo ni mbinu madhubuti katika ufundishaji. Zipo mada ambazo ni vigumu mwanafunzi kuzielewa endapo atafundishwa darasani kinadharia tu.

Katika baadhi ya shule za sekondari kwa mfano, walimu wanalazimika kufundisha mada za Sayansi, utafiti na upimaji (Jiografia) bila vitendo. Kufundisha kwa namna hiyo ni vigumu kwa mwanafunzi kuelewa. Mwalimu pia analazimika kutumia muda mrefu na juhudi kubwa ili wanafunzi waelewe.

Si rahisi mwanafunzi kuelewa bila kuona hali halisi. Mwanafunzi anajifunza vizuri kupitia milango yake ya fahamu kama macho, pua, masikio, ulimi na ngozi. Katika upimaji mwanafunzi anatakiwa ajue kupima urefu, pembe, vitu ambavyo si rahisi kuvielewa bila kufanya kwa vitendo.

Ili kufundisha kwa vitendo, wakati mwingine mwalimu na wanafunzi wanalazimika kufanya ziara ili kuyafikia maeneo ambako tafiti na upimaji unaweza kufanyika. Baadhi ya walimu hushindwa kusafiri kwa kuwa shule zao hazina pesa. Hata hivyo, ubunifu unahitajika katika kufundisha kwani mazingira yanayozunguka shule yanaweza pia kutumika kutoa mifano kwa baadhi ya masomo.

Mwanafunzi anayejifunza kwa vitendo na kufanya majaribio anaelewa vizuri kuliko anayesoma kinadharia. Nashauri Wizara ya Elimu na Utamaduni itoe kipaumbele kwa kununua vifaa vya kufundishia mada za utafiti na upimaji katika somo la Jiografia. Vilevile ijenge maabara zenye vifaa maalum kwa ajili ya kufundishia masomo ya Sayansi. Bila hivyo wanafunzi wataishia kukariri kuliko kuelewa kwa kina masomo hayo.

Vitabu vya Kiingereza viendane na mazingira yetu

Rukia Kimaro, SLP 5347, Tanga

Uhaba wa vitabu vya kufundishia somo la Kiingereza unasababisha walimu kutafuta vingine ili wasipoteze vipindi. Inatokea kuwa baadhi ya vitabu hivyo vinavyotumiwa kufundishia watoto vinafuata mitaala na mazingira ya nje ya nchi.

Mathalan, utakuta mifano ya matunda au vifaa vinavyotajwa ndani ya vitabu hivyo havipatikani nchini au katika mazingira aliyopo mwanafunzi! Kama mwana jamii anayejali elimu, nilibahatika kutembelea moja ya shule za msingi hapa mkoani Tanga na kuthibitisha hali hiyo. Lengo la kutembelea shule hiyo lilikuwa ni kufahamu changamoto wanazopata walimu na wanafunzi katika kufundisha na kujifunza somo la Kiingereza.

Baadhi ya walimu walieleza kuwa hawakuwa na vitabu maalum vya kufundishia. Vitabu walivyotumia kufundisha Kiingereza haviendani na mazingira na utamaduni wa kitanzania.

Ili kuondoa tatizo hilo, nashauri watunga mitaala wawashirikishe walimu na wanafunzi katika kuandaa vitabu vya kufundishia somo hilo. Maudhui ya vitabu hivyo yaendane na mazingira ya shule zetu hapa nchini na kuzingatia mila na desturi za watanzania.

Hiyo itamsaidia mwanafunzi si kujifunza Kiingereza pekee bali pia kufahamu mila, desturi na namna ya kukabiliana na maisha ya baadae kulingana na mazingira yanayomzunguka.

Notisi za kufundishia ni muhimu kuliko andalio la somo

M. Sunday, SLP 361, Bariadi

Baadhi ya walimu wa shule za msingi huko Bariadi wanaiomba Wizara ya Elimu na Utamaduni kufuta matumizi ya daftari la andalio la somo. Wanasema kwamba matumizi ya daftari hilo yanampunguzia mwalimu muda wa kusoma, kutafuta zana za kufundishia na kubuni mbinu za kufundishia.

“Kazi ya kufundisha haiwezi kufanyika bila mwalimu kujiandaa vizuri,” alisema mwalimu mmojawapo na akasisitiza kuwa si muhimu mwalimu kutumia muda mwingi kujaza katika kitabu cha andalio kuliko kusoma vitabu na kuandika notisi za kufundishia.

Walimu hao waliokuwa wakitoa maoni yao kwa nyakati mbalimbali walisisitiza kuwa andalio la somo halibebi ujumbe/hoja halisi. “Kinachoandikwa ndani ya daftari hilo hakimsaidii mwanafunzi hata mwalimu mwenyewe,” mwalimu mwingine aliongeza.

Kutokana na hali hiyo baadhi ya walimu wamekuwa wakitumia notisi za zamani kwa kukosa muda wa kuandaa notisi mpya zinazoendana na mabadiliko mbalimbali. Walimu hao waliishauri Wizara iwaruhusu kubaki na jukumu la kuonyesha maazimio ya kazi. “Huo ndio mwongozo halisi wa kazi kwa muhula au mwaka mzima,” walisisitiza.

Kwa kuwa daftari hubeba kilicho muhimu kwa mwanafunzi na mwalimu, walishauri kuwa mwalimu anapojisomea na kuandaa notisi; aandike vidokezo muhimu atakavyotumia wakati wa kufundisha. “Mkazo unapowekwa katika kujaza kitabu cha andalio, mwalimu anafundisha tofauti na alivyojiandaa,” mmoja wao alisema, na kusisitiza kuwa matumizi ya daftari la notisi yataleta mabadiliko makubwa kwa walimu na wanafunzi pia.

Tunahitaji walimu wenye taaluma si Kiingereza tu

Benedict Maembe, SLP 14837, Arusha

Baadhi ya wananchi wanapenda watoto wao wasome kwenye shule binafsi za msingi. Wana imani kuwa shule hizi zinatoa elimu bora zikilinganishwa na shule za umma. Shule hizi, zenye majina kama ‘Academy’, ‘English Medium’ ama ‘International Schools’ zinafundisha kwa lugha ya Kiingereza.

Tofauti na matarajio ya wazazi, hapa Arusha walimu ambao wanafundisha katika baadhi ya shule hizi hawana taaluma ya ualimu. Uwezo wa kuongea Kiingereza vizuri ndio kimekuwa kigezo cha kupata ajira ya kufundisha. Kwa hali hii, wanafunzi hawapati elimu inayolingana na malipo ya ada kubwa.

Baadhi ya ‘walimu’ hao hawana ushirikiano mzuri na wazazi. Haya yote yanatokana na ‘walimu’ hao kutoelewa umuhimu wa uhusiano mzuri kati ya mzazi na mwalimu. Kwa kuwa hawakusomea ualimu, walimu hao pia hawafundishi vizuri darasani kitendo ambacho kinawaathiri zaidi wanafunzi wasio na uwezo wa kuelewa kwa haraka. Wanazingatia maslahi binafsi kama kufundisha ‘tuisheni’ ili kujiongezea kipato.

Ni wajibu na muhimu kwa mzazi kupata taarifa za maendeleo ya mtoto wake kitaaluma, kinidhamu, kiafya na hata katika mambo mengine yanayofanyika nje ya darasa. Ushirikiano kati ya walimu na wazazi utamwezesha mtoto kupata elimu pamoja na kukuza vipaji alivyo navyo.

Nawashauri wamiliki wa shule hizi waajiri walimu wenye sifa na taaluma ya ualimu. Vilevile wakaguzi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni pia wapitie shule hizi mara kwa mara ili kunusuru watoto ambao ni taifa la kesho.

Shule za dini ziongeze ushindani katika elimu

Anderson Miti, SLP 663, Songea

Nafarijika kuona ongezeko la shule nchini. Hiyo inaashiria kuwa watanzania wanathamini elimu. Madhehebu ya dini mbalimbali pia yanazidi kuongeza idadi ya shule zake.

Nawapongeza wamiliki pamoja na walimu katika shule hizo kwa kuendeleza maadili mema ya dini kwa watoto wetu. Dini ni imani muhimu katika maisha ya watu. Uhuru wa kuabudu ni haki ya kikatiba ya kila mwananchi. Ndio maana Serikali ikaruhusu kuwepo kwa vipindi vya dini shuleni.

Shule za Serikali pia zinaheshimu imani za wanafunzi wa dini mbalimbali. Zipo shule zinazofundisha somo la dini ambalo linatahiniwa katika mitihani ya Taifa. Naamini kuwa mwanafunzi mwenye uwezo wa kufaulu katika somo la dini, anaweza pia kufaulu katika masomo mengine.

Baadhi ya shule zimekuwa zikilenga zaidi katika kutoa mafundisho ya dini. Sipendezwi kuona wanafunzi wengi kutoka baadhi ya shule za kidini wanafeli katika mitihani mingine ya kitaifa na kufaulu dini pekee. Hivyo nawashauri wanafunzi katika shule za kidini wasome kwa bidii katika masomo mengine pia.

Kwa upande mwingine nazipongeza shule za kidini ambazo wanafunzi wake wamekuwa wakifaulu vizuri. Nawashauri walimu wa shule za dini waige kutoka kwenye shule zinazofundisha vyema ili kuinua ubora wa elimu.

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukrani kwa PANOS kwa picha na kwa wote walioandaa habari zilizochapishwa katika jarida hili.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa HakiElimu.

Mhariri Mkuu: Rakesh Rajani

Timu ya *SautiElimu*
Lilian R. Kallaghe, Nyanda Shuli na Grace Frederick

Tuandikie!

HakiElimu, ***SautiElimu***
S.L.P. 79401
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (022) 2151852 au 3
Faksi: (022) 2152449
Baruapepe: media@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISSN 1821 5076

© HakiElimu, 2005

Ukurasa wa 2